## WASILIANA NASI


*Makao Makuu*

North East Tanzania Conference
P. o. Box 315, Same - KLM

*Idara ya Mawasiliano*

modaofpeace@gmail.com
+255 718 834 621

*Mtandaoni*

netc.adventistafrica.org


North East *Tanzania Conference*

# NJOZI YA KUANZISHA
# STUDIO




DESIGNED BY
NETC MEDIA



# "KUANZA KWA NETC MEDIA"

Tanzania ni moja kati ya nchi zinazokua kwa kasi kubwa katika suala zima la matuizi ya mbinu za kisasa za mawasiliano. Ikiwa na wakazi milioni 59, tayari inawatu wapatao milioni 23 ambao tayari wanatumia Internet kwa shughuli za mawasiliano. Hii ni sawa na kusema: 38.9% ya walengwa wa injili tayari ni watumiaji wa mbinu za kisasa za kimawasiliano. Huu ni mdokezo au kiashiria kimoja tu kati ya vingi, vinavyotuambia kwamba ni saa ya Kanisa kutumia mbinu za kisasa katika kufanya shughuli zake za kiutume za kuwafikia watu. Kusudi la Studio hii ni kupanua wigo wa injili na kuifikia idadi kubwa ya watu wanaotumia mbinu za kisasa za mawasiliano, ikiwemo Internet, Runinga, Redio na nyingine nyingi.

Andiko hili fupi limelenga kugusia mambo kadhaa ambayo yatafanywa na Studio hii kusudiwa.

**Utume wa Kanisa la Waadventista wa Sabato ni kuwaita watu wote wawe wanafunzi wa Yesu, kutangaza Injili ya milele katika muktadha wa Ujumbe wa Malaika watatu wa Ufunuo 14:6-12, na kuandaa ulimwengu marejeo ya Kristo yaliyo karibu.**



**Idara ya mawasiliano huhamasisha utumiaji wa programu thabiti ya uhusiano na mbinu zote za kisasa za mawasiliano, tekinolojia endelevu na vyombo vya habari katika kueneza injili.**

Mwongozo wa kanisa (toleo 2010) uk 104



Studio itakayoanzishwa NETC imekusudiwa kurahisisha, kuharakisha na kuboresha shughuli za kiutume katika Konferensi huku ikiwa sehemu ya vyanzo vya mapato ktk NETC

# "KWA NINI MEDIA?"

Ukizingatia Falsafa ya Idara ya Mawasiliano, ambayo ni kuwafikia watu kwa kutumia nyezo zote za kisasa za kimawasiliano, utagungua kuwa hawa watu 23,000,000 ambao tayari wanatumia njia ya kisasa kabisa ya Kimawasiliano, tayari ni Kondoo wa Yesu wanaosubiri na kugonja Mhubiri awaletee habari njema huko hewani.... kweli mavuno ni mengi kama alivyosema Yesu katika kitabu cha Luka 10:2

## Kondoo Milioni 23 Wako Mtandaoni Wanausubiri Mhubiri, Lakini ataendaje asipopelekwa?

## KUMEKUWA NA ONGEZEKO LA 26% KWA WATUMIAJI WA MAWASILIIANO YA MTANDAO KATI YA 2010 - 2017

10% Ya Watanzania kila siku hutumia Mitandao ya kijamii, kwa shughulu kadha wa kadha

## *Ulimwengu wa Karne ya 21* unahitaji mbinu za karne ya 21









## Wajibu wa Viongozi Chini ya Usimamizi wa Mchungaji

01. Kulielimisha Kanisa juu ya umuhimu wa Media/Studio ktk Utume
02. Kulikumbusha Kanisa kuwa tarehe ya sadaka imekaribia
03. Kuweka mkakati wa jinsi ya kulifikia Goli la Kanisa
04. Kuhakikisha kuwa sadaka hii inatolewa kwa kuwekwa ndani ya bahasha na kila mshiriki anapata risiti yake.
05. Kuhakikisha kuwa sadaka hii inaanza kutolewa mapema ili tarehe 27 Oktoba 2018 iwe kilele cha program hii.

# Faida Kuu Nne Ambazo Kila Mshiriki Anapaswa Kuzifahamu

Mambo ya Kiroho



Uinjilisti Madhubuti




Kazi za Kiofisi



Pato la Kanisa



# Mambo ya Kiroho



Moja kati ya vitu amabavyo media itasaidia ni kurahisisha kazi ya kujifunza mafundisho ya Biblia. Ni jambo lisilopingika kwamba hata katika kanisa la Bwana, wapo watu ambao bado hawajakomaa kimafundisho. Kama tungalimsimamisha kila mmoja wa waumini wa Kanisa, na kumuomba atufafanulie na kuchambua fundisho moja moja la Imani za Msingi, ingalibainika wazi kwamba watu wengi hawajazama na kukomaa katika kujifunza neno.

Media ni jibu sahihi kabisa kwa tatizo hili. DVD au Video moja moja yenye mafundishoya Biblia inaweza kuandaliwa mara moja lakini ikasambaa bila kujali mipaka ya kimazingira au mipaka ya kubanwa na wakati. Itaingia majumbani mahali pasipo hitaji ratiba wala kukutana na mchungaji, itatatazamwa kwenye magari mahali pasipo na uhitaji au ulazima wa uwepo wa fanani (mtoa mada), itafanya kazi toka nyumba moja mpaka nyumba nyingine ikiwa na ujumbe ule ule na msisitzo ule ule ambao mtu anaweza kuusikiliza tena na tena na tena.

Media itakuwa na kazi kubwa tena ya muhimu sana katika kuimarisha maisha ya kiroho; Biblia inasema "uwatakase kwa ile kweli neno lako ndiyo kweli" (Yoh 17:17), Kuna uwezekano mkubwa kwamba maisha ya waumini wengi Kanisani wanaishi maisha dhaifu kiimani kwa sababu majumbani mwao wamejaza video zinazoelezea mambo ya vita, uchawi, mauaji na mienendo mingine isiyozipendeza mbingu. Kwa kuliweka neno la Mungu majumbani mwetu kwa wingi tutachangia kuimarisha maisha ya mshiriki mmoja mmoja na hivyo kuliimarisha Kanisa. Lakini pia njia hii ya kujifunza maandikiko itawaimarisha watu na kuwafanya kudumu kanisani. Huenda baadhi ya watu wanatoka kanisani kwa sbabu ya uelewa finyu na kutokukomaa katika maandiko matakatifu; watu wa Mungu watakamilishwa wawe awe kamili, watakamilishwa ili wapate kutenda matendo mema kwa kuwa neno lina uwezo wa kutuimarisha 2 Timotheo 3:17.




# Uinjilisti Madhubuti



Wapendwa wa Bwana, hakuna jambo linaloleta furaha mbinguni kama kuwaleta kondoo wa Kristo katika zizi wanalopaswa kuishi ndani yake. Hakuna jambo lolote ambalo mwanadamu anaweza kufanya katika kuifanya mbingu ifurahi isipokuwa hili. Yesu alisema katika Luka 15:7: "...kutakuwa na furaha mbinguni kwa ajili ya mwenye dhambi mmoja atubuye." Mbingu zitafurahishwa sana Studio kwani itatusaidia kulitimiza hili kwa njia rahisi na iliyo ufanisi katika suala zima la kuifikia idadi kubwa ya watu ndani ya muda mfupi zaidi kuliko njia tulizozizoea.

Katika miaka 115 ya injili iliyopita, imekadiriwa kwamba katika NETC tume-kuwa 82,079 kutokana na njia mbalimbali ambazo zilitumiwa na watumishi wa Mungu katika kutafuta raia wa Ufalme wa Mungu. Hiyo ni sawa na wastani wa Ubatizo wa watu 714 kwa kila mwaka. Roho moja inathamani sana machoni pa Bwana, lakini pia roho maelfu zitaleta shangwe kuu machoni pa Mungu wetu. Linganisha wastani huo na a Mahubiri ya Runinga ya mwaka 2018 yaliyoitwa Ufunuo wa Matumaini ambapo watu 3,308 wali-batizwa. Hii inatuonesha kuwa kazi tuliyoifanya Bila Studio kwa miaka 115 ya Injili iliyopita, kutokana na mbinu za kimawasiliano inaweza kufanyika kwa wastani wa Miaka 5. Sio kwa sababu waliotangulia hawakuwa na juhudi bali kwa sababu Studio inaweza kuwafikia watu wengi zaidi kwa muda mfupi sana kwa kiwango kile kile cha juhudi za kutafuta Kondoo wa Yesu waliopotea.

Kwa mujibu wa takwimu za mwaka 2012 NETC inawakazi 6,804,000 na kwa kuwa takwimu za mwaka 2018 zinaonesha kwamba 80% ya Watanzania wanapokea habari kwa kupitia njia ya Internet (Bila kuhusisha njia nyingine za mawasiliano), tunao uhakika wa kuwafikia Watu 5,443,200.

Ukweli ni kwamba, Media (Vyombo vya Habari) ndiyo njia sahihi kwa wakati huu ya kufanya Uinjilisti Madhubuti.

# Kazi za Kiofisi



Moja kati ya changamoto ambazo wachungaji wa mitaa na Wakurugenzi watakutana nazo ni namna ya kufanya semina za kila idara kwa kila kanisa tena kwa manufaa ya kiutendeji yanayotokana na semina kufika kwa wakati. Wakati mwingine imemlazimu Mchungaji kutumia njia ya kuwakusanya viongozi wote kwa pamoja ili kuwafanyia semina za warsha huku tukiwa tumealika wakufunzi toka maeneo mbalimbali maana mchungaji akiwa mwenyewe hawezi, lakini bado njia hii inaleta gharama kubwa kwani watu wanapaswa kusafiri na kuahirisha baadhi ya shughuli huku wakitumia gharama kubwa katika kufika eneo la mkutano na kupata malazi na chakula. Pamoja na hayo bado kutoa semina toshelevu kwa wakati mwafaka imekuwa changamoto kwa Wakurugenzi na wachungaji kutokana na ratiba zinazoshuka kutoka ngazi za juu za Kanisa. Wakati mwingine semina zimewafikia walengwa kwa kuchelewa (katikati ya mwaka) tayari kazi nyingi zilizopaswa kufanywa kwa namna flani bora, zikiwa zimekosewa. Studio hii itakuwa suluhisho kwa jambo hilo.

Video moja ya semina inapo tengenezwa na mchungaji mmoja au mkurugenzi kwa ngazi ya konferensi anayetaka kusisitiza malengo flani ya kazi kwa kipindi flani cha muda wa uongozi, hatakuwa na haja ya kuzunguka kila mahali; na wakati akiandaa semina hiyo wachungaji wengine wataendelea na kazi nyingine za kanisa na huduma kwa waumini. Si vema wachungaji wote wa mitaa yote ya konferensi kushughulika na kazi iyo hiyo moja kwa wakati huo huo wakati tungaliweza kumpa mtu mmoja aifanye na kuimaliza kwa wakati mfupi kabisa na gharama nafuu zaidi. DVD itaukomboa wakati (Waefeso 5:16, Wakolosai 4:5) kwa kwenda kila eneo kusudiwa ndani ya muda mfupi sana, badala ya mkufunzi kwenda katika kila kituo na kila kanisa kwa semina iyo hiyo, jambo ambalo limekuwa na gharama kubwa sana na kuchukua muda mrefu zaidi.

Kazi kubwa na muda mwingi utatumika katika utekelezaji na usimamiaji wa maelekezo ambayo yamekwenda upesi tena kwa haraka katika makanisa. Ulimwengu wa sasa ni ulimwengu unaokwenda kasi na sisi kama kanisa la Bwana, tena tunaotamani ujio wa Yesu uwe wa haraka kama ahadi yake ilivyo, tunapaswa kwenda na kasi hii na hivyo kuwa na Studio si jambo linalopaswa kucheleweshwa.

# Pato la Kanisa




Moja kati ya mambo muhimu sana katika kukamilisha utume wa Kanisa ni pamoja na taasisi zinazofanya kazi za kiutume kuwa na uwezo wa kujiendesha na kutoa mahitaji muhimu kwa wale wanaofanya kazi ndani ya taasisi hizo. Na hivyo ni jambo lenye baraka kwa Kanisa kuwa na miradi inayoweza kulipatia Kanisa pesa kwani kazi nyingi za utume zinahitaji fedha ili ziweze kutekelezeka. Wafanyakazi wanahitaji kulipwa, wachungaji wanahitaji kulipwa, studio itahitaji kujiendeleza hapo baadaye kwa kuendelea kununua vifaa vya kisasa zaidi, safari zitafanyika ili kuzalisha kazi za Studio.

Kila jambo jema na zuri linahitaji gharama flani ili liweze kufanyika. Katika mahubiri ya Ufunuo wa Matumaini mwaka 2018 tulihitaji angalau Bilioni 1 hivi ili kufanikisha mahubiri. hivyo suala la utume na kipato cha fedha ni vitu visivyoweza kutenganishwa.

Huu ni mfano tu, wa pato tunaloweza kupata kutokana na Studio tutakayoianzisha kwa mwaka mmoja tu.

| PROGRAM | IDARA | MAKADIRIO YA WANUNUAJI | | BEI @ DVD | JUMLA |
|---|---|---|---|---|---|
| | | *MAKANISA* | *BINAFSI* | | |
| **Semina** | Huduma | 200 | 500 | 20,000 | 14,000,000.00 |
| | Shule ya Sabato | 200 | 500 | 20,000 | 14,000,000.00 |
| | Mawasiliano | 200 | 500 | 20,000 | 14,000,000.00 |
| | Wanawake | 200 | 500 | 20,000 | 14,000,000.00 |
| | Watoto | 200 | 500 | 20,000 | 14,000,000.00 |
| | Uwakili | 200 | 500 | 20,000 | 14,000,000.00 |
| | Vijana | 200 | 500 | 20,000 | 14,000,000.00 |
| | Maofisa | 200 | 500 | 20,000 | 14,000,000.00 |
| **Imani ya Msingi** | DVD 1 | 200 | 500 | 10,000 | 7,000,000.00 |
| | DVD 2 | 200 | 500 | 10,000 | 7,000,000.00 |
| | DVD 3 | 200 | 500 | 10,000 | 7,000,000.00 |
| | DVD 4 | 200 | 500 | 10,000 | 7,000,000.00 |
| | DVD 5 | 200 | 500 | 10,000 | 7,000,000.00 |
| **Masomo ya Unabii** | Series 1 | 200 | 2000 | 5,000 | 11,000,000.00 |
| | Series 2 | 200 | 2000 | 5,000 | 11,000,000.00 |
| | | | | ***Jumla Kuu Kabisa*** | **169,000,000.00** |